JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

Simu Na: +255 (026) 2963309/13/14
Nukushi: +255 (026) 2963316
Barua Pepe: ps@lands.go.tz
Tovuti: www.lands.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
2 Mtaa wa Ardhi,
S.L.P. 2908,
**40477 DODOMA.**

## TAARIFA KWA UMMA

## USIMAMIZI WA UTEKELEZAJI WA MIPANGO YA UENDELEZAJI MIJI NCHINI

07 Agosti 2026

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia vyombo mbalimbali vya Habari imeona juhudi za Mheshimiwa Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam katika kuhakikisha kuwa wamiliki wa ardhi wanaendeleza maeneo yao kwa kuzingatia vibali vya ujenzi vinavyotolewa na Halmashauri.

Wizara inapongeza hatua zinazoendelea kuchukuliwa katika kusimamia utekelezaji wa vibali ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam lengo likiwa ni kuhakikisha wamiliki wa ardhi wanazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Ardhi hasa katika uendelezaji wa maeneo wanayoyamiliki.

Aidha, Wizara inapenda kuwajulisha wananchi wote kuwa, kwa mujibu wa **Fungu la 38 (1 & 2) la Sheria ya Ardhi (Sura ya 113),** kila mmiliki wa ardhi aliyepewa nyaraka ya Haki ya Kumiliki Ardhi, anapaswa kutekeleza sharti la uendelezaji wa ardhi yake na pale maendelezo hayo yanapokuwa ni ujenzi wa majengo, mmiliki anatakiwa kuhakikisha anaomba kibali cha ujenzi kwa mujibu wa Sheria ya Mipangomiji Sura 355 na masharti ya mipango ya uendelezaji iliyoandaliwa na kuidhinishwa katika maeneo husika.

Hivyo, naelekeza wamiliki wote wa ardhi kuzingatia masharti ya uendelezaji ardhi. Serikali itaendelea kuchukua hatua stahiki kwa wale watakaoshindwa kutekeleza masharti ya uendelezaji.

Wizara itashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kukagua uendelezaji unaofanyika katika Mkoa wa Dar es Salaam na maeneo mengine yote nchini ili kuhakikisha uendelezaji unazingatia vibali vya ujenzi vilivyotolewa.

Dkt. Leonard Akwilapo (Mb.)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**